HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

Tarehe 14 Julai 2017

Mh. Mwenyekiti
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango,
Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe

YAH: MREJESHO WA BAJETI YA HALMASHAURI KWA SHUGHULI ZA MAENDELEO NA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2017/2018 BAADA YA KUIDHINISHWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO NA OFISI YA RAIS -TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR – TAMISEMI)

UTANGULIZI
Mh . Mwenyekiti;

Bajeti ni muhimu kwa taasisi yoyote ili iweze kutekeleza malengo ya kuundwa kwake; umuhimu huo ni pamoja na:-

- Bajeti ni chombo cha kutekeleza sera za nchi na yale yanayotazamiwa kufanyika kwa muda uliopangwa na gharama zinazohusika.
- Bajeti ni chombo cha uwajibikaji kwa kuweka wajibu kwa watu wanaohusika na usimamizi wa fedha na programu mbalimbali.
- Bajeti ni chombo cha kutoa mwelekeo wa uchumi kwa vile hutoa viwango vya uwekezaji rasilimali, kudhibiti matumizi katika umma na viwango vya upatikanaji wa fedha na matumizi ya serikali.

Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ibara ya 135 – 139) pamoja na sheria za serikali za mitaa (Na. 7 na Na.9 za mwaka 1982 na marekebisho ya Na.6/1999) inasisitiza kuandaa na kutekeleza Mipango na Bajeti zinazokidhi vipaumbele vya wananchi waishio katika Halmashauri kwa muda muafaka.

Mh. Mwenyekiti,

Halmashauri imezingatia sheria hizi na mchakato wa maandalizi ya bajeti hii umezingatia taratibu zinazotakiwa kufuatwa na serikali za mitaa katika utayarishaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2017/2018 – 2019/2020

MAANDALIZI YA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

***Mh* . Mwenyekiti;**

Bajeti ya Halmashauri ya mwaka 2017/2018 – 2019/2020 imeandaliwa kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa, Miongozo hiyo ni pamoja na :

I. Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025
II. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya mwaka 2015 -2020
III. Malengo ya Maendelo Endelevu (Sustainable Development Goals)

***Mh*. Mwenyekiti**

Aidha bajeti hii imezingatia vipaumbele toka kwa jamii iliyoibuliwa kwa kutumia mbinu shirikishi ya fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) pamoja na mpango mkakati ambao Halmashauri imejiwekea.

***Mh*. Mwenyekiti**

Miongozo hiyo imefafanuliwa kama ifuatavyo:

i. Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; ambayo ina malengo yafuatayo

- Kuwaletea wananchi maisha bora na mazuri
- Kuwa na uongozi bora na utawala wa kisheria
- Kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani
- Jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi
- Amani, utulivu na umoja.

ii. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya mwaka 2015 -2020

Ilani inaeleza yafuatayo;

- Mafanikio ya kiuchumi na kijamii
- Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea
- Kuboresha sekta za uzalishaji mali
- Kuimarisha sekta za miundo mbinu na huduma za kiuchumi
- Kuendeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi
- Kuboresha sekta ya huduma za jamii

MALENGO YA HALMASHAURI

***Mh*. Mwenyekiti;**

Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe imeandaa na kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia malengo muhimu kwa Halmashauri ndani ya kipindi husika. Malengo hayo ni pamoja na;

1. Kupunguza maambukizi ya UKIMWI na kuboresha utoaji wa huduma.
2. Kuimarisha na kuendeleza Mkakati wa kitaifa wa kupambana na kuzuia rushwa
3. Uboreshaji wa hali ya maisha na huduma za jamii.
4. Kuboresha huduma za Kiuchumi, kuongeza kipato na kuimarisha miundombinu.
5. Kuimarisha Utawala bora na uwajibikaji katika ngazi zote.
6. Utunzaji endelevu wa maliasili na mazingira.
7. Kuhakikisha kuwepo kwa Usawa wa kijamii , kijinsia, kuwawezashaji na kuwashirikisha wananchi katika kujiletea maendeleo yao.
8. Kudhibiti na kupunguza madhara ya maafa na majanga yanayoweza kutokea na kusababisha upotevu wa maisha na uharibifu wa mali.

Mh. Mwenyekiti

Katika kuhakikisha huduma za msingi zinatolewa kwa wananchi Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe katika mwaka 2017/2018, imeweka mikakati kadhaa ili kuboresha huduma hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

i) Kujenga na Kukamilisha miundombinu ya miradi ya maji safi na salama kwa wananchi.

ii) Kuboresha miundo mbinu ya elimu na Kusimamia utoaji taaluma katika shule za msingi na sekondari na kuwawezesha wanafunzi wa darasa la VII kufaulu mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi kwa asilimia 100% na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza.

iii) Kuboresha huduma za afya Kwa kukarabati na kujenga majengo ya kutolea huduma za afya, kuboresha upatikanaji wa madawa na kuongeza wataalamu wa kutoa huduma.

iv) Kuboresha miundombinu ya barabara kwa kufanyia matengenezo na kujenga madaraja ya kudumu.

v) Kuchangia na kuhamasisha miradi inayo ibuliwa na kutekelezwa na jamii yenyewe.

vi) Kuboresha na kuendeleza Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.

vii) Kushirikiana na jamii katika kusimamia raslimali za maliasili na kuzitumia kwa njia endelevu.

viii) Kuhamasisha akina mama na vijana kujiimarisha kiuchumi kupitia vikundi vidogo vidogo

Mh. Mwenyekiti,

Baada ya mchakato wa Bajeti mwaka 2017/2018, kupitiwa katika vikao mbalimbali ngazi ya Mkoa na Wizara, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe imeidhinishiwa jumla ya Tshs. 31,633,722,460 ambapo

fedha kwa ajili ya matumizi ya shughuli zisizo za Maendeleo ni kiasi cha Tshs. 18,844,487,000.00 zikijumuishaTshs. 949,350,000.00 za matumizi ya kawaida na Tshs. 17,895,137,000.00 za mishahara kwa maeneo ya Ruzuku. (Fedha toka Serikali kuu), kiasi cha Tshs. 1,284,487,505.00 kwa maeneo yasiyo ya Ruzuku (Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri) zimeelekezwa kwa shughuli zisizo za maendeleo ambapo kiasi cha Tshs. 682,935,200.00 kwa matumizi ya kawaida na Tshs. 21,656,800.00 kwa ajili ya mishahara na Tshs. 110,167,505.00 Michango ya Jamii katika vituo vya kutolea huduma wanapokwenda kupata matibabu.

Kwa upande wa shughuli za Maendeleo, kiasi cha Tshs. 11,504,747,955.00 kikijumuisha jumla ya Tshs. 4,404,972,000.00 fedha toka serikali kuu (Vyanzo vya Ndani), Tshs. 6,679,775,955.00 toka kwa wafadhili mbalimbali, Tshs. 489,300,000.00 Mchango wa Halmashauri katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo toka vyanzo vyake vya ndani and Tshs. 420,000,000.00 ni mchango wa jamii (nguvu kazi na vifaa vya ujenzi) katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa ni kama unavyoonekana katika majedwali yanayofuata;

Jedwali Na.1: Mgawanyo wa fedha za Ruzuku toka Serikali kuu mwaka 2017/2018 kwa kila Idara

KASMA NDOGO	IDARA/KITENGO (MAELEZO)	MISHAHARA (Tshs)	GPG (Tshs)	MATUMIZI YA MENGINEYO (OC)	JUMLA
500A	Utawala na Utumishi	2,401,298,200.00	44,025,000.00	43,577,000.00	2,488,900,200.00
500A	Mishahara kwa VEO'S	483,000,000.00	0	0	483,000,000.00
501A	Mazingira Uendeshaji	0	6,000,000.00	0	6,000,000.00
502E	Baishara na Masoko	0	6,000,000.00	0	6,000,000.00
503 (A – D)	Mipango	0	9,000,000.00	0	9,000,000.00
506D	Ushirika	0	6,000,000.00	0	6,000,000.00
512 (F, G & H)	Maliasili	0	6,000,000.00	0	6,000,000.00
512 (A, C & D)	Ardhi	0	6,000,000.00	0	6,000,000.00
515A	Ukaguzi wa Ndani	0	9,000,000.00	0	9,000,000.00
519B	Ufugaji Nyuki	0	6,000,000.00	0	6,000,000.00
527A	Maendeleo ya Jamii	0	6,000,000.00	0	6,000,000.00
	Jumla Ndogo	***2,884,298,200.00***	***104,025,000.00***	***43,577,000.00***	***3,031,900,200.00***
505 (A & B)	Mifugo na Uvuvi	159,732,000.00	0	9,759,640.00	169,491,640.00
	Jumla Ndogo	***159,732,000.00***	***0.00***	***9,759,640.00***	***169,491,640.00***
506B	Kilimo na Umwagiliaji	220,071,000.00	0	14,044,360.00	234,115,360.00
	Jumla Ndogo	***220,071,000.00***	***0.00***	***14,044,360.00***	***234,115,360.00***
507A	Elimu Msingi - Utawala	111,783,000.00	0	4,252,000.00	116,035,000.00
507B	Elimu Msingi - Uendeshaji	7,979,952,000.00	0	347,764,000.00	8,327,716,000.00
	Jumla Ndogo	***8,091,735,000.00***	***0.00***	***352,016,000.00***	***8,443,751,000.00***
508A	Mganga Mkuu	92,328,000.00	0	21,928,400.00	114,256,400.00
508D	Vituo vya Afya	494,664,000.00	0	43,740,000.00	538,404,000.00
508E	Zahanati	1,410,816,000.00	0	80,630,600.00	1,491,446,600.00
508F	Afya - Kinga	201,792,000.00	0	1,090,000.00	202,882,000.00
	Jumla Ndogo	***2,199,600,000.00***	***0.00***	***147,389,000.00***	***2,346,989,000.00***
509A	Elimu Sekondari	4,176,116,800.00	0	248,428,000.00	4,424,544,800.00
	Jumla Ndogo	***4,176,116,800.00***	***0.00***	***248,428,000.00***	***4,424,544,800.00***
510A	Maji Vijijini	52,236,000.00	0	13,193,000.00	65,429,000.00
	Jumla Ndogo	***52,236,000.00***	***0.00***	***13,193,000.00***	***65,429,000.00***
511A	Ujenzi	111,348,000.00	0	16,918,000.00	128,266,000.00
	Jumla Ndogo	***111,348,000.00***	***0.00***	***16,918,000.00***	***128,266,000.00***
	JUMLA KUU 1	***17,895,137,000.00***	***104,025,000.00***	***845,325,000.00***	***18,844,487,000.00***

Jedwali Na 2: Mgawanyo wa fedha za Mapato ya Ndani mwaka 2017/2018 kwa Idara/Kitengo

KASMA NDOGO	IDARA/KITENGO	MISHAHARA (Tshs)	MATUMIZI MENGINEYO (Tshs)	JUMLA
500A	Utawala	21,656,800.00	338,759,200.00	360,416,000.00
500B	Utumishi	0	15,000,000.00	15,000,000.00
501C	Mazingira	0	4,072,000.00	4,072,000.00
502 (A, B&D)	Fedha na Biashara	0	181,500,000.00	181,500,000.00
503A	Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji	0	25,572,000.00	25,572,000.00
505A	Mifungo na Uvuvu	0	4,072,000.00	4,072,000.00
506A	Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji	0	19,072,000.00	19,072,000.00
508A	Mganga Mkuu		13,000,000.00	13,000,000.00
512 (C & E)	Ardhi	0	2,036,000.00	2,036,000.00
512F	Maliasili	0	2,036,000.00	2,036,000.00
514A	Sheria	0	7,000,000.00	7,000,000.00
515A	Ukaguzi wa Ndani	0	4,072,000.00	4,072,000.00
516 (A & B)	Manunuzi	0	15,000,000.00	15,000,000.00
517B	Uchaguzi	0	15,500,000.00	15,500,000.00
518A	TEHAMA	0	20,100,000.00	20,100,000.00
527A	Maendeleo ya Jamii	0	4,072,000.00	4,072,000.00
519A	Ufugaji Nyuki	0	12,072,000.00	12,072,000.00
	JUMLA KUU 2	***21,656,800.00***	***682,935,200.00***	***704,592,000.00***

Jedwali Na.3: Mchanganuo wa fedha za Miradi ya Maendeleo mwaka 2017/2018 – Fedha toka Serikali Kuu

NA	CHANZO CHA FEDHA/PROGRAMU	Fedha za Ndani (TShs)	Fedha za Nje (TShs)	Jumla (TShs)
1	LGDG – CDG (HSDG, DADPS, CDG)	971,659,800.00	0	971,659,800.00
2	LGDG - CBG	107,962,200.00	0	107,962,200.00
3	MFUKO WA JIMBO	42,592,000.00	0	42,592,000.00
4	MFUKO WA BARABARA	1,828,250,000.00	0	1,828,250,000.00
5	KENDELEZA ELIMU - SEKONDARI	0	335,484,000.00	335,484,000.00
6	Rural Water Supply and Sanitation Program (RWSSP)	0	3,607,817,000.00	3,607,817,000.00
7	National Multisectoral Strategic Fund - NMSF	0	54,009,000.00	54,009,000.00
8	Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF)	0	472,811,000.00	472,811.00
9	UNICEF	0	371,110,000.00	371,110,000.00
10	UJENZI WA JENGO LA OFISI	700,000,000.00	0	700,000,000.00
11	Tanzania Social Action Fund (TASAF)	0	1,093,880,955.00	1,093,880,955.00
12	Global Fund		24,664,000.00	24,664,000.00
13	WORLD BANK		720,000,000.00	720,000,000.00
14	ELIMU BURE - MSINGI	506,190,000.00	0	506,190,000.00
15	ELIMU BURE - SEKONDARI	248,318,000.00	0	248,318,000.00
	JUMLA KUU 3	***4,404,972,000.00***	***6,679,775,955.00***	***11,084,747,550.00***

Jedwali Na.4: Mchanganuo wa fedha za Mapato ya Ndani kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo mwaka 2016/2017

Na	CHANZO CHA FEDHA	Fedha za Ndani (TShs)	Fedha za Nje (TShs)	JUMLA (TShs)
1	Mchango wa Halmashauri katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo	469,728,000.00	-	469,728,000.00
2	Mchango wa Jamii katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo (Vifaa vya Ujenzi)	420,000,000.00	-	420,000,000.00
	JUMLA KUU 4	***889,728,000.00***	***0***	***889,728,000.00***

Mh. Mwenyekiti

Pamoja na majedwali hayo yanayoonesha mgawanyo wa fedha toka vyanzo mbalimbali kwa matumizi mengineyo na shughuli za miradi ya maendeleo kwa kila idara/kitengo, majedwali yafuatayo yanaonesha miradi ya maendeleo ambayo Halmashauri itatekeleza katika mwaka 2017/2018.

A: FEDHA ZA MFUKO WA MAPATO YA NDANI

1: IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI - MFUKO WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuziwezesha serikali za vijiji kusimamia shughuli za maendeleo	234,864,000.00	Mapato ya ndani ya Halmashauri	Vijiji 108 na Kata 21
	JUMLA	**234,864,000.00**		

2: IDARA YA ELIMU MSINGI - MFUKO WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha uchangiaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayopitiwa na mwenge wa Uhuru	4,000,000.00	Mapato ya ndani ya Halmashauri	Maeno yenye miradi itakayopendekezwa
	JUMLA	**4,000,000.00**		

3: IDARA YA ARDHI NA MALIASILI - MFUKO WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha zoezi la Upimaji wa viwanja na Uandaaji wa Ramani za Mipango Miji	27,254,000.00	Mapato ya ndani ya Halmashauri	Igwachanya, Ilembula, Mtewele na Wanging'ombe
2	Kuwezesha zoezi la uthamini wa majengo ya makazi na biashara pamoja na majengo ya serikali yaliyokamilika	10,716,000.00	Mapato ya ndani ya Halmashauri	Kata zote 21
	JUMLA	**37,970,000.00**		

4: IDARA YA ARDHI NA MALIASILI - MFUKO WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha Halmashauri kufanya usajiri wa vikundi vya Kiuchumi vya Wanawake na Kutoa mikopo yenye masharti nafuu	52,500,000.00	Mapato ya Ndani ya Halmashauri	Makao Makuu ya Halmashauri na Maeneo yatakayokuwa na vikundi
2	Kuwezesha Usimamizi wa vikundi vilivyopatiwa mikopo na kufanya ufuatiliaji wa mikopo kwenye vikundi vya wanawake viliyopewa mikopo	6,216,000.00	Mapato ya Ndani ya Halmashauri	Maeneo yatakayokuwa na vikundi
3	Kuwezesha Halmashauri kufanya usajiri wa vikundi vya Kiuchumi vya Vijana na Kutoa mikopo yenye masharti nafuu	52,500,000.00	Mapato ya Ndani ya Halmashauri	Makao Makuu ya Halmashauri na Maeneo yatakayokuwa na vikundi
4	Kuwezesha Usimamizi wa vikundi vilivyopatiwa mikopo na kufanya ufuatiliaji wa mikopo kwenye vikundi vya Vijana viliyopewa mikopo	6,216,000.00	Mapato ya Ndani ya Halmashauri	Maeneo yatakayokuwa na vikundi
	JUMLA	**117,432,000.00**		

5: IDARA YA AFYA - MFUKO WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha uanzishwaji wa Hospitali ya Wilaya	35,000,000.00	Mapato ya Ndani ya Halmashauri	Wilaya ya Wanging'ombe
2	Kuwezesha Halmashauri kulipia gharama za ujenzi wa mradi wa Kituo cha Afya Mdandu	40,462,000.00	Mapato ya Ndani ya Halmashauri	Kijiji cha Mdandu, Kata ya Mdandu
	JUMLA	**75,462,000.00**		
	JUMLA KUU MAPATO YA NDANI	**469,728,000.00**		

B: FEDHA ZA MFUKO WA RUZUKU KWA SERIKALI ZA MITAA – UWEKEZAJI (CDG)

1: IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI -MFUKO WA RUZUKU KWA SERIKALI ZA MITAA

NA	MIRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MIRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha zoezi la Maandalizi na uwasilishaji wa Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2018/2019	12,600,000.00	LGDG - CDG	Makao Makuu ya Halmashauri
2	Kuwezesha zoezi la Usimamizi na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo	35,639,600.00	LGDG - CDG	Kata zote 21 za Halmashauri
3	Kuziwezesha Kamati za Maedeleo za Kata (WDC), kubaini na kutumia rasilimali za zilizopo katika maeneo yao kwa ajili ya kupanga Mipango na Bajeti	53,981,100.00	LGDG - CDG	Makao Makuu ya Halmashauri
4	Kuwezesha Halmashauri kukusanya na kuchambua takwimu kwa ajili ya maandalizi ya Wasifu wa Uwekezaji wa Halmashauri	5,741,500.00	LGDG - CDG	Makao Makuu ya Halmashauri
	JUMLA	**107,962,200.00**		

2: IDARA YA ELIMU MSINGI - MFUKO WA RUZUKU KWA SERIKALI ZA MITAA (LGDG)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa	9,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Itandula, Kata ya Wanging'ombe
2	Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa	9,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Mambegu, Kata ya Luduga
3	Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa	9,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Ilovi, Kata ya Makoga
4	Ukamilishaji wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa	9,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Mwilamba, Kata ya Kipengere
5	Ukamilishaji wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa	9,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Idunda, Kata ya Kipengere
6	Ujenzi wa chumba 1 cha darasa	9,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Wangamiko, Kata ya Malangali
7	Ujenzi wa chumba 1 cha darasa	9,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Kanamalenga, Kata ya Ilembula
8	Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa	11,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Banawanu, Kata ya Udonja
9	Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa	11,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Lutegelo, Kata ya Wangama
10	Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa	11,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Ihanzutwa, Kata ya Itulahumba
11	Ukarabati wa vyumba 2 vya madarasa	11,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Uhenga, Kata ya Uhenga
12	Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa	10,658,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Makondo, Kata ya Saja
13	Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa	11,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Wangutwa, Kata ya Uhambule
14	Ujenzi wa chumba 1 cha darasa	11,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya msingi Mkeha, Kata ya Uhambule
	JUMLA	**139,658,000.00**		

3: IDARA YA ELIMU SEKONDARI - MFUKO WA RUZUKU KWA SERIKALI ZA MITAA (LGDG)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Ujenzi wa daharia (Hostel)	28,000,000.00	LGDG - CDG	Shule ya sekondari Usuka
2	Ukamilishaji wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa	10,000,000.00	LGDG -CDG	Shule ya sekondari Philip Mangula
3	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa	20,000,000.00	LGDG -CDG	Shule ya sekondari Igosi
4	Ukamilishaji wa ujenzi wa Bwalo (Dinning Hall)	20,000,000.00	LGDG -CDG	Shule ya sekondari Igwachanya
5	Ukamilishaji wa ujenzi wa daharia (Hostel)	28,000,000.00	LGDG -CDG	Shule ya sekondari Kijombe
6	Ukamilishaji wa ujenzi wa Bwalo (Dinning Hall)	28,000,000.00	LGDG -CDG	Shule ya sekondari Makoga
7	Ukamilishaji wa ujenzi wa Hostel shule ya sekondari Wanike	20,000,000.00	LGDG -CDG	Shule ya sekondari Wanike
	JUMLA	**154,000,000.00**	LGDG -CDG	

4: IDARA YA KILIMO , UMWAGILIAJI NA USHIRIKA - MFUKO WA RUZUKU KWA SERIKALI ZA MITAA (LGDG)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Ujenzi wa Kituo cha kukusanyia nyanya	15,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Mtewele, Kata ya Uhambule
2	Ukarabati wa jengo la soko	22,000,000.00	LGDG - CDG	Ilembula
3	Ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Maonesho ya wakulima na wafugaji	25,000,000.00	LGDG - CDG	Viwanja vya maonesho ya Nane Nane, Mbeya
	JUMLA	**62,000,000.00**		

5: IDARA YA AFYA - MFUKO WA RUZUKU KWA SERIKALI ZA MITAA (LGDG)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Katenge
2	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	15,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Mhaji
3	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	15,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Ng'anda
4	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Kanamalenga
5	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Mng'elenge
6	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Samaria
7	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Ivigo
8	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Itambo
9	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Mtapa
10	Ukamishaji wa ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Utiga
11	Kusaidia ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Gonelamafuta
12	Kusaidia ujenzi wa jengo la wodi	13,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Imalinyi
13	Kusaidia ujenzi wa jengo la wodi	13,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Wangama
14	Kusaidia ujenzi wa jengo la wodi	13,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Isindagosi
15	Kusaidia ujenzi wa jengo la zahanati	19,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Kipengere
16	Ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba ya mtumishi	17,000,000.00	LGDG - CDG	Zahanati ya Uhenga
17	Ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba ya mtumishi	17,000,000.00	LGDG - CDG	Zahanati ya Banawanu
18	Ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya	33,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Luduga, Kata ya Luduga
19	Ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya	28,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Mdandu, Kata ya Mdandu
20	Ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya	33,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Saja, Kata ya Saja
21	Ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya	33,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Igagala, Kata ya Ulembwe
22	Kusaidia ujenzi wa Kituo cha Afya	32,039,600.00	LGDG - CDG	Kata ya Ilembula
23	Ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya	33,000,000.00	LGDG - CDG	Kijiji cha Palangawanu, Kata ya Igwachanya
24	Kusaidia ujenzi wa Kituo cha Afya	23,000,000.00	LGDG - CDG	Kata ya Uhambule
	JUMLA	**508,039,600.00**		

6: IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI - MFUKO WA RUZUKU KWA SERIKALI ZA MITAA (CBG)

NA	MIRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuendesha mafunzo ya siku 2 juu ya ukusanyaji wa Takwimu, uchambuzi na utunzaji waKumbukumbu kwa Maafisa Watendaji wa Kata ba Vijiji	12,040,000.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
2	Kuwezesha kuendeshwa kwa kikao cha tathimini ya hali ya ukusanyaji wa mapato na rasilimali za utekelezaji wa miradi katika mazingira ya utekelezaji	20,352,990.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
3	Kuendesha mafunzo ya siku 1 kwa Wenyeviti wa vijiji na Maafisa Wtendaji wa Vijiji juu ya utunzaji wa kumbukumbu, uongozi bora ba ukusanyaji wa Mapato	16,190,000.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
4	Kuendesha mafunzo ya siku 1 kwa Waheshimiwa madiwani juu ya Usimamizi na Ufuatilaiji wa miradi ya Maendeleo	12,328,660.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
5	Kuendesha mafunzo ya siku 2 kwa Wakuu wa Idara na Vitengo juu ya Taratibu za Manunuzi, Usimamizi wa Fedha za Umma na Ujazaji wa OPRAS	9,720,000.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
6	Kuwezesha watumishi wa Idara za Utumishi na Fedha kuhudhuria mitihani ya ujuzi	10,340,000.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
7	Kuwezesha usimamizi na utoaji wa huduma sahihi katika mfumo wa taarifa za kiutumishi	9,300,000.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
8	Kuwezesha Usimamizi na ufuatiliaji wa uendeshaji wa serikali za vijiji na Kamati za Maendeleo ya Kata	6,894,330.00	LGDG - CBG	Vijiji na Kata
9	Kuwezesha mazingira ya utendajaji kazi kuwa salama na ya uhakika kwa kuwepo na vitendea kazi	10,796,220.00	LGDG - CBG	Makao Makuu ya Halmashauri
	JUMLA	**107,962,200.00**		

C: FEDHA TOKA SERIKALI KUU – VYANZO VINGINE

1. ELIMU MSINGI NA SEKONDARI - FEDHA ZA ELIMU BURE

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha shule za msingi kuwa na mazingira mazuri kwa wanafunzi kujifunza na walimu kufundisha	506,190,000.00	ELIMU BURE FUND	Shule 107 za msingi
2	Kuwezesha shule za sekondari kuwa na mazingira mazuri kwa wanafunzi kujifunza na walimu kufundisha	248,318,000.00	ELIMU BURE FUND	Shule 16 za Sekondari
	JUMLA	**754,508,000.00**		

2: IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI - FEDHA ZA RUZUKU TOKA SERIKALI KUU

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo inaendelea kutekelezwa ndani Jimbo	42,592,000.00	MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO	Kata zote 21
2	Ujenzi wa jengo la Ofisi za Halmashauri kwa awamu ya Tatu	500,000,000.00		Makao Makuu ya Halmashauri
3	Ujenzi wa nyumba za wakuu wa Idara	200,000,000.00		Makao Makuu ya Halmashauri
	JUMLA	**742,592,000.00**		

D: FEDHA ZA PROGRAMU YA USAMBAZAJI WA MAJI VIJIJINI NA USAFI WA MAZINGIRA -WSDP

1: IDARA YA MAJI - PROGRAMU YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA (SANITATION)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kufanya mafunzo elekezi kwa wakusanyaji takwimu za msingi za hali ya Afya na Usafi wa mazinfira	4,730,400.00	Benki ya Dunia	Kata za Igwachanya, Itulahumba na Uhambule
2	Kufanya utafiti wa awali utakaowezesha kuanzishwa kwa mfumo bora wa takwimu za Hali ya Afya na Usafi wa Mazingira	7,730,000.00	Benki ya Dunia	Kata za Igwachanya, Itulahumba na Uhambule
3	Kuwezesha uendeshwaji wa zoezi la uchefuaji kwa jamii	11,479,600.00	Benki ya Dunia	Kata za Igwachanya, Itulahumba na Uhambule
4	Kuwezesha kuenndeshwa kwa mashindano ya Usafi wa mazingira ngazi ya vijiji na kata	3,280,000.00	Benki ya Dunia	Vijiji 86 kwenye kata za Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira
5	Kufanya Usimamizi na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira	5,150,000.00	Benki ya Dunia	Kata za Igwachanya, Itulahumba na Uhambule
6	Kufanya ukaguzi wa kina wa hali ya Afya na Usafi wa mazingira katika vituo vya Kutolea huduma za Afya	2,630,000.00	Benki ya Dunia	Vituo 45 vya kutolea huduma za Afya
	JUMLA	**35,000,000.00**		

2: IDARA YA MAJI - PROGRAMU YA USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI

NA	MIRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MIRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha Usajiri na utoaji wa mafunzo kwa Jumuiya za Watumia Maji	3,813,000.00	Benki ya Dunia	Makao Makuu ya Halmashauri na maeneo yenye miradi ya maji
2	Ujenzi wa mradi wa maji ya bomba	510,016,000.00	Benki ya Dunia	Vijiji vya Uhenga, Ukomola, Saja, Mapogoro and Igomba
3	Ujenzi wa mradi wa maji mtiririko	959,491,000.00	Benki ya Dunia	Vijiji vya Igando na Kijombe
4	Ujenzi wa mradi wa maji mtiririko	947,011,000.00	Benki ya Dunia	Kijiji cha Mtapa
5	Ukamilishaji wa mradi wa maji mtiririko	260,000,000.00	Benki ya Dunia	Kijiji cha Kinenulo
6	Kuwezesha Usimamizi na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Maji	47,730,000.00	Benki ya Dunia	Makao Makuu ya Halmashauri na maeneo yenye miradi ya maji
7	Kumwezesha Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri kufanya Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji	1,552,500.00	Benki ya Dunia	Maeneo yenye miradi ya Maji inayotekelezwa
8	Kuwezesha maandalizi ya mchoro na usanifu wa mradi wa bwawa	104,000,000.00	Benki ya Dunia	Wilaya ya Wanging'ombe
9	Upanuzi wa mradi wa maji wa mtiririko wa Igosi	260,000,000.00	Benki ya Dunia	Kata ya Igosi
	JUMLA	**3,093,613,500.00**		

E: FEDHA ZA UNICEF

1: IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha Usimamizi na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo	15,260,000.00	UNICEF	Kata zote 21
	JUMLA	**15,260,000.00**		

2: IDARA YA ELIMU MSINGI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuendesha kikao cha robo mwaka cha tathimini ya hali ya ufundishwaji wa wanafunzi wa darasa la I na II	21,644,000.00	UNICEF	Makao makuu ya Halmashauri
2	Kuwezesha Waratibu Elimu wa Kata kufanya Usimamizi na Ufuatilaiji wa Programu ya ufundishaji wa mtaala mpya wa K3	21,400,000.00	UNICEF	Kata zote 21
3	Kuendesha mafunzo elekezi kwa maafisa elimu ya msingi, MEK na walimu wakuu juu ya masuala ya kijinsia na kuwalinda watoto	20,870,000.00	UNICEF	Shule za msingi
4	Kuendesha mafunzo ya siku saba juu ya ushauri na unasihi kwa masuala ya ukatili wa kijinsia, UKIMWI na utoaji wa taarifa za hali ya ukatili wa kijinsia na ukatili kwa watoto	38,470,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halamshauri
5	Kuendesha mafunzo ya siku mbili kwa wakufunzi wa masuala ya ukatili dhidi ya watoto na mawasiliano yake	13,790,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halamshauri
6	Kuendesha mafunzo ya siku tatu kwa walimu toka shule 20 juu ya Programu ya TUSEME na mchakato wake pamoja na uanzishwaji wa Vilabu wezeshi katika shule za msingi	19,050,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halamshauri
7	Kuendesha mafunzo kwa siku mbili kwa wallimu 107 na waratibu elimu kata juu ya namna bora ya kuhudumia na kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum	38,906,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halamshauri
	JUMLA	**152,486,000.00**		

3: IDARA YA AFYA

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuendesha mafunzo ya siku 5 kwa watoa huduma za Afya juu ya MIYCAN	18,000,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
2	Kufanya Usimamizi elekezi juu ya masuala ya Lishe kwa vituo vya kutolea huduma za Afya na kwa jamii	18,250,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
3	Kuendesha mikutano ya kila robo ya Kamati ya Lishe ya Halmashauri	2,960,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
4	Kuendesha zoezi la uchambuzi na uhakiki wa takwimu katika kikao cha mwaka	2,420,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
5	Kuendesha mafunzo ya siku 3 kwa watoa huduma za Afya juu ya ukuaji na usimamizi wa ukuaji wa watoto katika masuala ya lishe	12,705,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
6	Kuefanya usimamizi na ufuatiliaji na marejeo ya Programu ya PMTCT na RMNCH kwa kutumia malengo yaliyowekwa	8,695,000.00	UNICEF	Vituo vya kutolea huduma
7	To conduct quartely intergrated (MNCH, PMTCT, IVD) supportive supervision/mentoring	28,250,000.00	UNICEF	Vituo vya kutolea huduma
8	Kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya kila mwezi ya narejeo ya "District Maternal and Perinatal, Death Surveilence (MPDSR)"	12,525,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
9	Kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya vituo vya kutolea huduma za Afya juu ya masuala ya "Maternal New born Quality Improvement (QI)	13,325,000.00	UNICEF	Vituo vya kutolea huduma
10	Kusaidia utekelezaji wa Mpango kazi wa "Maternal Newborn Quality Improvement (QI)" wa kituo cha kutolea huduma za Afya	14,150,000.00	UNICEF	Vituo vya kutolea huduma
11	Kuendesha semina elekezi kwa ajili ya utekelezaji wa "MNH Champion Program" kwa vikundi 20	13,325,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
12	Kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa "MNH Champion Program" katika kata husika	4,250,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
13	Ununuzi wa vifaa maalum kwa ajili ya KMC	17,440,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
14	Kuendesha uchambuzi na marejeo ya takwimu na viashiria vya RMNCH toka mifumo ya DHIS2 na HMIS	1,470,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
15	Kuendesha mkutano wa siku 1 wa waratibu wa masuala ya lishe katika NGOs/CBOs kwa ajili ya kuandaa Mpango wa mwaka 2018/2019 wa masuala ya lishe	1,240,000.00	UNICEF	Makao Makuu ya Halmashauri
	JUMLA	**169,005,000.00**		

F: FEDHA ZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuendesha mikutano ya uhamasishaji na kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa jamii kupima afya zao kujua hali zao katika maambukizi ya VVU	3,771,000.00	NMSF	Kata zote 21
2	Kuwezesha zoezi la kufanya utambuzi na tathimini ya wanafunzi wenye waishio mazingira hatarishi (MVC) kwa ajili ya kupatiwa msaada wa kielimu	14,500,000.00	NMSF	Shule zote za Sekondari na Msingi
3	Kusaidia vituo vinne vya kulelea wanafunzi yatima kwa msaada wa fedha kwa ajili ya mahitaji maalum kwa wanafunzi	8,000,000.00	NMSF	
4	Kutoa mafunzo kwa wajumbe 13 wa Kamati ya UKIMWI wilaya juu ya wajibu na majukumu yao	2,654,000.00	NMSF	Makao Makuu ya Halmashauri
5	Kumwezesha Mratibu wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI na watumishi wengine kufanya maandalizi ya Siku ya UKIMWI duniani	2,900,000.00	NMSF	Makao Makuu ya Halmashauri
6	Kumwezesha mratibu wa Mapambao dhidi ya UKIMWI kuhudhuria Semina, vikao na makongamano	2,004,000.00	NMSF	Makao Makuu ya Halmashauri
7	Kuwezesha maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mapambano dhidi ya UKIMWI	1,400,000.00	NMSF	Makao Makuu ya Halmashauri
8	Kuendesha kikao kazi cha kutoa maelekezo kwa watumishi juu ya sera na miongozo mbalimbali ihusuyo masuala ya UKIMWI	1,655,000.00	NMSF	Makao Makuu ya Halmashauri
9	Ununuzi wa "Computer"	2,000,000.00	NMSF	Makao Makuu ya Halmashauri
10	Kuwezesha uendeshwaji wa mikutano ya kila robo kujadili utekelezaji wa afua za Mapambano dhidi ya UKIMWI	5,125,000.00	NMSF	Makao Makuu ya Halmashauri
11	Kusaidia vikundi 20 vya WAVIU	10,000,000.00	NMSF	Kata zote 21
	JUMLA	**54,009,000.00**		

G: FEDHA ZA MFUKO WA PAMOJA WA AFYA (HSBF)

1: IDARA YA AFYA (HEALTH SERVICES)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha Usimamizi na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo	95,400,006.00	HSBF	Vituo vya Kutolea huduma za Afya
	JUMLA	**95,400,006.00**		

2: IDARA YA AFYA (HOSPITALI TEULE YA ILEMBULA)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuwezesha Hospitali Teule ya Ilembula kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi	66,869,833.00	HSBF	Hospitali Teule ya Ilembula
	JUMLA	**66,869,833.00**		

3: IDARA YA AFYA (COMMUNITY HEALTH INITIATIVES/PROMOTIN)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kufanya ushawishi na uhamasishaji kwa jamii juu ya kanuni za Afya bora, Usafi na kubadili mtazamo wao	22,000,000.00	HSBF	Kata zote 21
	JUMLA	22,000,000.00		

4: IDARA YA AFYA (VITUO VYA AFYA)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuviwezesha vituo vya Afya kutoa huduma kwa kupatiwa madawa na vifaa tiba	79,999,600.00	HSBF	Vituo vya Afya vyote
	JUMLA	**79,999,600.00**		

5: IDARA YA AFYA (ZAHANATI)

NA	MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA	CHANZO CHA FEDHA	ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI
1	Kuziwezesha Zahanati kutoa huduma kwa kupatiwa madawa na vifaa tiba	208,741,561.00	HSBF	Zahanati zote
	JUMLA	**208,741,561.00**		